In the name of Allaah, the Most Merciful,
the Bestower of Mercy

Maana ya saum

Saumu katika lugha ni kujizuia,Ama Saumu kwa upande wa sheria ni kumuabudu Allah kwa kujizuia na kula na kunywa na vyenye kufuturisha, kutoka alfajiri ya kweli hadi kuzama kwa jua.

NGUZO ZA SAUMU

1.Kunuia
2.Kujizuia na vyenye kufunguza

VIGAWANYO VYA NIA KWENYE SAUMU

1.Kunuia Saumu ya faradhi:Ni lazima kulala na nia usiku (kabla ya alfajiri),Na yatosha kufungamanisha nia kabla mwezi haujaingia,na kunuia ni moyoni na kutamka nia ni uzushi.
2.Nia kwa saumu ya sunna:yakubalika wakati wowote mchana pindi utakapokua hukutanguliza chenye kuharibu saumu yako,lakini ujira wake utaanza wakati aliponuia.

VIGAWANYO VYA SAUMU

1.Saumu ya lazima (Ramadhan ,Saumu za kafara na nadhiri)
2.Saumu za sunna

MASAHRTI YAKUWAJIBIKA KUFUNGA

1.Uisilamu
2.Kua na akili
3.Kubaleghe (Na anaekaribia kubaleghe anahimizwa kufunga na msimamizi wake)
3.Mkaazi wa mji -Si lazima kufunga kwa msafiri, na lilobora kwake ni kufunga (endapo hakutampa shida), na ni haraka kuondosha dhima,kupata wepesi, na fadhla za mwezi wa Ramadhan.
5.Kuwa mzima
6.Kuwa twahara kutokamana na hedhi ama nifasi

MARADHI NA SAUMU

Maradhi yako aina mbili:
1.Maradhi yasiyotarajiwa kupona, sawia na mzee asiyeweza kufunga, kwake si lazima kufunga ila hutoa vibaba viwili kulisha maskini, kila siku masikini mmoja.Au akusanye maskini kwa idadi ya zile siku awalishe mchana au usiku,au atoe chakula awape maskini kwa idadi ya siku alizofungua ,kila maskini mmoja nusu pishi (kilo moja na nusu ya chakula cha mji; kilichozoeleka). Na imependekezwa ampe na kitoweo atakachotolea kama nyama au Mafuta.
2.Maradhi yanaotarajiwa kupona isipokuwa yampa uzito kufunga akiwa mgonjwa, hukmu yake hukutanishwa na mwanamke akiwa kwenye ada yake ya mwezi au nifasi. Sawia na anayenyonyesha na msafiri. Anapaswa kulipa zile siku alizofungua akipona ,na akifa kabla yakupona husamehewa.

VYENYE KUTHIBITISHA KUINGIA KWA MWEZI WA RAMADHAN

Yafuatayo huthibitisha kuingia kwa mwezi wa Ramadhan;
1.kuonekana kwa mwezi wa Ramadhan.
2.kukamilika kwa sha'ban siku thalathini.

VYENYE KUFUNGUZA

1.Kula na kunywa kwa kukusudia ,Aliyesahau akanywa au akala, saumu yake iko sawa (Nahupewa udhuru kutojua na kusahau)
2.Kufanya tendo la ndoa , likitokea mchana wa Ramadhan na saumu kwake ni waajib yamlazimu kafara nzito, ambayo ni kuacha mtumwa huru, ikiwa hakupata basi afunge miezi miwili mfulilizo, ikiwa hakuweza alishe maskini sitini.
3.Kutokwa na manii kwa kukusudia iwe kwa utangulizi wa tendo la ndoa au kubusu au kukumbatia n.k
4.Ni kila chenye kuchukua mfano wakula ,kama sindano ya chakula. Aidha, ikiwa sindano ni ya dawa haiharibu.
5.Kutoa damu kwa hijama (kuumika).Ama kutoa damu nyepesi
kama, kupima damu- haiharibu.
6.Kujitapisha kwa kukusudia.
7.Kutoka damu ya hedhi.

YALIOPENDEKEZWA KWENYE SAUMU

1.Kula daku
2.Kuchelewesha daku
3.Kufanya haraka kuvunja saumu.
4.Kufturu kwa Rutwab (tende nyevunyevu), na sunna iwe witri. Ikiwa hakupata basi afungue kwa tende za kawaida, ,ikiwa hakupata apige tama la maji,na akikosa cha kufungulia nacho ,anuie kuwa amefungua moyoni.
5.Kuomba dua wakati wakuvunja saumu ,na akiwa kwenye saumu.
6.Afanye wingi wakutoa sadaka.
7.Kujitahidi na kuswali swala za usiku.
8.Kusoma Quraan kwa wingi.
9.Kufanya umrah.
10.Kusema "mimi nimefunga" kwa yule aliyemtukana
11.Kujitahidi kutafuta usiku wa cheo (Laylatul- Qadr)
12.Kukaa itikafu kumi la mwisho

YALIYOCHUKIZWA KWA ALIYEFUNGA

1.Kupitisha kiasi kwenye kusukutua na kutia maji puani.
2.Kuonja chakula pasipokuwa na haja.
Yaruhusiwa kwa aliefunga kumeza mate,kuonja chakula
kukihitajika, kuoga. kupiga mswaki,kujitia manukato

YALIYOHARAMISHWA KWA ALIYEFUNGA

1.Ni haramu kumeza makohozi na wala hayaharibu saumu.
2.Kubusu kwa yule ambae anahofia kuharibu saumu.
3.Kusema maneno ya uongo (nayo nikufanya kile cha haramu)
4.Ujinga (upumbavu, kutokuwa mpole)
5. Kuunganisha saumu (kutofungua kwa siku mbili au zaidi)

SAUMU ZA SUNNA

1.Kufunga siku sita katika mwezi wa shawal kwa aliyekamilisha Ramadhan.Na ubora ni kufuatisha , kuanzia mwezi pili , shawal.
2.Kufunga siku ya Arafa kwa ambaye hayuko hajj mwaka huo.
3.Kufunga siku ya A'shuraa, pamoja na mwezi tisa na kumi na moja.
4.Kufunga siku ya Alhamisi na juma tatu imekokotezwa.
5.Kufunga siku tatu kwa kila mwezi na ubora ziwe siku nyeupe (13 14 na 15).
6.Kufunga siko moja na kutofunga siku ya pili yake n.k.
7.Kufunga kwa wingi mwezi wa Muharram.
8.Kufunga siku tisa za mwezi Dhul-Hijja.
9.Kufunga sha'baan lakini asikamilishe

SAUMU ZILIZO CHUKIZWA

Kufunga siku za ijumaa , juma mosi na juma pili kwa upekee (bila kufungamanisha mojawapo na siku nyengine) .Lakini ikisadifiana moja ya siku hizo na siku ya A'rafat hakuna neno,kuifunga.

SAUMU ZILIZO HARAMISHWA

1.Kukhusishwa mwezi wa Rajab na saum.
2.Kufunga siku ya shaka ,ama yule ambae alikuwa na saumu akifunga aweza kufunga.
3.Kufunga siku za Eid mbili.
4.Kufunga siku za Tashrik (11, 12 ,13 Dhulhijja) isipokua kwa ambae hakupata mnyama wa hady (kichanjwa kwa anayefanya hijja pamoja na umra au akaanza na umra kisha akahitimisha kwa hijja).
5.Kufunga kila siku.
Imependekezwa kufuatanisha katika kulipa,Na inatakiwa kufanya haraka baada ya siku ya eid ,wala hairuhusiwi kuchelewesha hadi Ramadhani nyengine, akicheleweshа bila kulipa bila sababu hakuna kinacho mlazimu zaidi ya kulipa saumu hio isipokuwa ana dhambi la kuchelewesha

ZAKATUL FITR

Ina mlazimu muislamu ambaye yuko hai na jua lime zama siku ya mwisho ya mwezi wa Ramadhan na ana chakula ambacho kimezidi kwa matumizi yake mchana wa siku ya Eid na usiku wake, atjitolee Swa'a (pishi) ya chakula na kwa walioko chini yake na yoyote anayewajibika kwake kumlisha. Imependekezwa kumtolea mtoto alie tumboni.

NI IPI HIKMA YAKUTOA ZAKATUL FITRI

1.Kumtakasa aliyefunga na mambo au matendo yakipuuzi au machafu.
2.Kuwafanya wasiojiweza kutosheka na kutoomba siku ya Eid.

WAKATI WA KUTOA FITRI

1.wakati unaofaa ni kabla ya ya swala ya Eid kwa siku moja au mbili.
2wakati uliopendekezwa ,nao ni kabla ya swala ya eid baada ya swala ya alfajiri.
3.wakati waharamu kutoa,bada ya swala ya eid.

SWALA YA EID

Swala ya Eid ni wajibu kwa kila mtu,na huswaliwa pale jua likichomoza na kupanda hadi wakati wa zawal,wala halikupita wakti wake,na sunna kuswaliwa kwenye uwanja, nje ya jengo,na yafaa kuswaliwa msikitini,na mtu ale tende witri kabla ya swala na mtu aoge na kutia manukato na kuvaa mavazi mazuri aliyonayo na kurudi njia tofauti na ile uliyopitia wakati wakwenda .na hakuna neno kupongezena kwa kusema;

تقبل الله منا ومنكم
(Allah atutakabalie sisi na nyinyi).
Na ni sunna kuleta Takbir Mutlaq (ambazo hazikufungamanishwa na swala za faradhi,bali wakati wowote ule,kuanzia usiku wa Eid na vile vile Takbira baada ya swala za faradhi hadi jua kuzama siku ya Eid,Na sifa ya Takbir ni
الله أكبر ،الله أكبر،لاإله إلا الله ،والله أكبر ،الله أكبر ،الله أكبر ولله الحمد.

- Sifa ya swala ya Eid ni rakaa mbili kabla ya khutba.
- Inasomwa Takbira sita kwenye rakaa ya kwanza baada ya Takbira ya kufunga Swala.
- Baada ya kupiga Takbiir na kuinuka katika rakaa ya pili, utafuatisha na Takbiir tano zingine.

باللغة السواحلية

فقه الصيام

هيثم بن محمد جميل سرحان
المدرس بمعهد الحرم بالمسجد النبوي

www.alsarhaan.com